

»Kupandikiza mpunga«

Mavuno ya mchele ni mengi barani Afrika. Hata hivyo, mavuno yanaweza kuzidishwa iwapo wakulima watazingatia kanuni bora za usimamizi wa mpunga.

Kuna faida mbalimbali za kupandikiza mpunga ambazo ni pamoja na; kusababisha ukuaji wa haraka wa mimea, kurahisisha kupalilia kwa mazao, kuongeza mavuno, kutumia mbegu chache katika upanzi, na kuharakisha mchakato wa kuchagua mbegu. Hata hivyo, wakulima wanapaswa kupanga mapema shughuli za shambani kabla ya kupandikiza. Daima pandikiza miche kwenye kina cha 3cm kwa ajili ya kuotesha mizizi haraka, na hivyo kusababisha ongezeko la mavuno.

Shughuli za shambani

Hakikisha unatumia mbegu bora ili kupata miche yenyewe nguvu, lakini usipande mbegu nydingi kwenye kitalu kwani huku kunaweza kusababisha uotaji wa miche miembamba, ambayo itachukua muda mrefu kustawi vyema ili kupandikizwa.

Pia tayarisha shamba mapema kwa kusawazisha, na kulainisha udongo ili kurahisisha kupandikiza. Pandikiza siku 15–20 baada ya kupanda mbegu, wakati miche ina nguvu.

Hakikisha kuna kiwango kidogo cha maji kabla ya kupandikiza. Mwagilia kitalu kabla ya kung'oa miche ili kupunguza uharibifu wa mimea.

Baada ya kung'oa, pandikiza miche kwa haraka ili kuzuia miche kukauka. Hakikisha kwamba unapanda miche 1–3 kwa kila kilima ili kutoa matawi zaidi.

Daima hakikisha muachano ufaao kati ya mimea ili kurahisisha kupalilia na kuongeza mavuno.

Hatimaye, panda upya ndani ya wiki moja katika mahali ambapo

mbegu hazikuota ili kuhakikisha ukuaji sawa wa mimea.